**TAARIFA ZA MRADI WA KIWANDA KIDOGO CHA KUSINDIKA MAZIWA MOTHER DIARIES MAARUFU FULL MANYONYO KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU WILAYANI RUFIJI TAREHE 03/06/2017**

**Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru,** Ndg **Amour Hamad Amour**, naomba nichukue nafasi hii kukukaribisha wewe na msafara wako katika eneo hili la Mradi ili ujionee shughuli za Maendeleo ya wananchi.

**Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru,** huu ni mradi wa maziwa na ulianza Utekelezaji wake mnamo mwaka 2010 kwa ubia wa watu watatu wakiwemo wanawake wawili na mwanaume mmoja. Mradi huu ulianza na mtaji wa Tshs.20,000,000/=. Mpaka sasa thamani ya mradi ni Tshs. 260,000,000/=. Lengo la mradi huu ni kuongeza kipato kwa kuongeza thamani ya maziwa, kuongeza muda wa kukaa kwa bidhaa hiyo (shelf life) hivyo kuwa na soko la uhakika kwa kuuza maziwa. Mradi huu umehamishwa kutoka kwenye jengo la kukodi la mtu binafsi ambalo lilipitiwa na Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2016 na kiongozi wa mbio za mwenge kushauri tuone uwezekano wa kuwa na jengo tunalomiliki sisi wenyewe. Kwa hiyo jengo hili ni utekelezaji wa maagizo hayo.

**Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru,** kiwanda hiki kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha lita 3,000 za maziwa ya mgando kwa siku ukilinganisha na lita 900 zinazozalishwa kwa sasa.

Maziwa yanayozalishwa na kiwanda hiki huuzwa kwenye maeneo mbalimbali ndani ya wilaya ya Rufiji na maeneo ya nje ya Wilaya kama vile Dar es Salaam, Masasi, Kibiti, Mtwara na Lindi.

**Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru,** kiwanda hiki kitakapokamilika kitatoa ajira zaidi kuliko hivyo sasa ambapo kuna wafanyakazi 12, kati yao 5 ni ajira ya kudumu, na 7 wana ajira ya muda na takribani watu 65 ambao wana ajira isiyo rasmi ya kukusanya maziwa kwa ajili ya Kiwanda. Mipango ya baadae ni kuwa na ranchi ya mifugo ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa maziwa na kuwa sehemu ya mafunzo ya kuboresha mifugo na pia kujenga Kiwanda chenye Miundombinu rafiki kwa ajili ya usindikaji wa maziwa.

**Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru,** Pamoja na changamoto kadhaa tulizonazo, mradi huu una manufaa ya uzalishaji wa ajira na kipato kwa jamii na pia tunalipa kodi kwa Serikali.

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Tunakuomba utuwekee jiwe la msingi katika mradi wetu wa Kiwanda cha maziwa.***

***"MWENGE OYEE", IKWIRIRI KUSINI OYEE!***

***TUNYWE MAZIWA KWA AFYA ZETU!***

***SOMOYE HASSAN CHAMBO***

**TAARIFA YA MRADI WA JENGO LA UPASUAJI KATIKA KITUO CHA AFYA IKWIRIRI KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2017 WILAYANI RUFIJI TAREHE 03.06.2017**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Ikwiriri Wilayani Rufiji kukupongeza wewe na msafara wako kwa kazi kubwa ya kuukimbiza mwenge wa Uhuru. Sisi wananchi wa Ikwiriri tunayo furaha kuupokea Mwenge huu katika Mji wetu wa Ikwiriri. Mbele yako ni mradi wa Jengo la upasuaji. Mradi huu umekamilika na umegharimu jumla ya **Tshs.180,000,000.00** zilizohusisha ujenzi na ununuzi wa vifaa tiba. Kati ya hizo, Tshs. **100,000,000.00** zilitolewa na wahisani mbalimbali na Tshs. **80,000,000.00** zimetolewa na Halmashauri. Jengo hili limegawanyika katika sehemu zifuatazo; Mapokezi, Sehemu ya kubadilishia nguo kwa wanawake na wanaume, Sehemu ya kunawa mikono kabla na baada ya upasuaji, Chumba cha upasuaji, Chumba kwa ajili ya kupunguza uchafu wa vifaa na nguo, Chumba kwa ajili ya utakasaji, Chumba cha mapumziko baada ya upasuaji na Chumba cha Daktari kwa ajili ya Mganga Mkuu wa Kituo.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Manufaa ya mradi huu ni kutoa huduma kwa mama wajawazito kutoka maeneo ya Mohoro, Ikwiriri na maeneo ya jirani hivyo kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga. Jumla ya mama wajawazito 1,140 wanatarajiwa kunufaika na huduma hii kwa mwaka. Kwa ujumla inakadiriwa kuwa zaidi ya watu 53,000 watanufaika na huduma ya afya kupitia majengo haya ikitiliwa maanani kuwa majengo haya yako katika barabara kubwa inayotoka mikoa ya kaskazini kwenda mikoa ya kusini.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017, karibu utufungulie mradi wetu wa Jengo la upasuaji katika kituo chetu cha Afya.

***"MWENGE OYEE"***

***IKWIRIRI OYEE! AFYA OYEEEE!***

***Dr. IDD RAJAB MALINDA***

***MGANGA MFAWIDHI***

**TAARIFA FUPI YA MRADI WA KIWANDA KIDOGO CHA KIKUNDI CHA USEREMALA MKONGONI IKWIRIRI KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2017**.

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa, Ndugu **Amour Hamad Amour**; Karibu sana Ikwiriri wewe pamoja na msafara wako.

Mbele yako ni Kikundi cha Useremala cha vijana Mkongoni ambao tumejiunga kwa pamoja ili kuunganisha nguvu zetu kwa kuongeza mtaji pamoja na kujiongezea kipato.

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge Mradi huu umeanza tarehe 01/01/2000 ukiwa na wanachama waanzilishi 40, mpaka sasa kikundi kina wanachama 48 na wanaojifunza 18. Kikundi chetu kina akaunti **Na. 21310007107 KIKUNDI CHA MKONGONI NMB** Kibiti.

Mradi huu una thamani ya Jumla ya Tsh **20,000,000.00** ikiwa ni nguvu zetu sisi wenyewe.

Aidha tunapenda kuishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kwa kuwa tumekuwa na ushirikiano mzuri na wamekuwa pamoja nasi kwa kutupa ushauri na hata kutuwezesha kwa njia ya mkopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambapo kwa mwaka 2015/2016 tuliweza kupata mkopo wa Tsh 2,000,000.00 na tumewezeshwa kupata kazi ya kutengeneza madawati yapatayo 50 yenye thamamani ya Tsh 8,250,000.00. Madawati haya hatujayakamilisha na pia mkopo hatujarejesha kutokana na Serikali kusimamisha shughuli za uzalishaji wa bidhaa za misitu kwa zaidi ya miezi sita kuanzia Septemba 2016 hadi Februari 2017. Kwa kuwa sasa zuio hilo limeondolewa, tumajipanga kumaliza *"order"* za wateja, kulipa mikopo na kumalizia kazi ya kutengeneza madawati ya Halmashauri kabla ya Julai 2017.

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge, Kikundi na jamii kwa ujumla kimenufaika na ajira kwa vijana, vijana kupata mafunzo na kupunguza ukaaji wa kwenye vijiwe ambapo tungeathirika na uzururaji na matumizi ya madawa ya kulevya.

Tunaiomba Serikali iendelee kutuwezesha mikopo yenye riba nafuu ili tuweze kuboresha maisha yetu na kulipa ushuru na kodi.

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge, kwa heshima na taadhima tunakuomba ukague mradi wetu.

***"Mwenge Oyee"***

***"UWEZESHAJI WA VIJANA OYEE"***

***ATHUMANI YUSUF MSANGU***

***KATIBU MSAIDIZI WA KIKUNDI***

**TAARIFA YA MRADI WA UJENZI WA SHULE MPYA YA MSINGI YA SHAURIMOYO KATIKA KIJIJI CHA NYAMWAGE KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2017 WILAYANI RUFIJI TAREHE 03.06.2017**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Kwa niaba ya wananchi wa Kijiji cha Nyamwage hususani kitongoji cha Shaurimoyo tunayo furaha kuupokea Mwenge wa Uhuru katika shule yetu ya Shaurimoyo. Tunakukaribisha wewe binafsi pamoja na msafara wako wote unaouongoza katika kufanikisha Mbio za Mwenge wa Uhuru 2017.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, hadi kufikia hatua hii, shule hii ina jumla ya madarasa 4, ofisi 1 na vyoo matundu 4. Shule ina walimu 5, wanafunzi 469 na ilisajiliwa mwaka 2015 kwa namba PW/05/02/116. Mwaka huu 2017 shule inatarajia kufanya mtihani wa kwanza wa darasa la nne. Kuanzishwa kwa shule hii kulitokana na hitaji la wananchi wenyewe kutokana na adha waliyokuwa wakiipata watoto wao kufuata elimu umbali mrefu wa km.7 hadi Nyamwage. Ujenzi wa shule hii umegharimu jumla ya shilingi **69,976,400** kwa kuchangiwa kama ifuatavyo:-

- Mchango wa Nguvu za wananchi Tshs. 1,500,000.00
- Wawekezaji katika kijiji cha Nyamwage Tshs. 63,476,400.00
- Mchango wa Halmashauri (W) Tshs. 5,000,000.00

**JUMLA** Tshs. **69,976,400.00**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Manufaa ya kuanzishwa kwa shule hii kumewarahisishia watoto wengi waliokuwa wakisafiri umbali mrefu kwenda kutafuta elimu na hivyo kupunguza utoro kwa kiwango kikubwa. Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017, karibu utuzindulie shule yetu ya Shaurimoyo.

***"MWENGE OYEE"***

***SHAURIMOYO OYEE!***

***ELIMU OYEEEE!***

***"FURAHIA ELIMU YAKO, SIO DAWA ZA KULEVYA"***

***Mikidadi Kiwanjani Kilindo***

***MWALIMU MKUU***

***SHULE YA MSINGI SHAURIMOYO***

## TAARIFA YA MRADI WA MAJI WA MBWARA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE MWAKA 2017

**Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge,** sisi wananchi wa kijiji cha Mbwara tunayo furaha kuupokea Mwenge wa Uhuru katika kijiji chetu ambapo ifuatayo ni taarifa ya ujenzi wa mradi wetu wa maji wa Mbwara.

**Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge,** Mradi wa maji Mbwara ni miongoni mwa Miradi iliyotekelezwa chini ya progamu ya Maji na Usafi wa mazingira uliofadhiliwa na Benki ya Dunia.Mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo mwezi Octoba 2013 na kukamilika mwezi Januari 2015 na kukabidhi kwa kamati ya maji inayoendesha mradi chini ya usimamizi wa Serikali ya Kijiji. Ujenzi wa mradi huu ulijumuisha kazi zifuatazo;1. Ujenzi wa Tangi la maji lenye ukubwa wa mita za ujazo 25, 2. Ununuzi na ulazaji wa bomba kuu la maji kutoka kisimani hadi tangini lenye urefu wa mita 3,651.3. Ununuzi na ulazaji wa mabomba ya kusambazia maji ya saizi mbalimbali yenye urefu wa mita 5,262, Ujenzi wa vituo vya kuchotea maji, Ujenzi wa nyumba ya pampu, Ununuzi na ufungaji wa Jenereta, Ununuzi na ufungaji wa pampu ya kuvuta maji.

Kazi zote hizi zimegharimu fedha za kitanzania kiasi cha shilingi **215,373,700/=** kutoka Benki ya Dunia na nguvu za wananchi ni Shilingi **2,000,000/=**. Hivyo jumla ya mradi ni shilingi **217,373,700/=.** Hata hivyo katika siku za karibuni, mradi huu ulisimama kutokana na kuungua kwa mota. Kwa sababu hiyo Halmashauri ya Wilaya imetoa Tshs.**4,000,000.00** kwa ajili ya kununulia mota mpya na hivyo kutatua tatizo na kurejesha huduma ya maji.

**Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge,** Mradi huu unahudumia watu wapatao **4,365.** Katika siku za nyuma wananchi wa kijiji hiki walikuwa wanatumia muda mwingi kutafuta maji hivyo muda huo unatumika kuongezea kipato katika familia.

**Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge,** Kupitia kwako tunaiomba Halmashauri itusaidie kubadilisha mfumo wa umeme wa dizeli na kuwa umeme wa TANESCO ili shughuli za uendeshaji wa pampu ziweze kufanyika kwa gharama nafuu.

***Ndugu kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru mwaka 2017,***

***Tunakuomba utuzindulie mradi wetu wa maji wa Mbwara.***

***"Mwenge Oyee"***

***Baraka Mwinje***

***Afisa Mtendaji wa Kijiji***

***Kijiji cha Mbwara***

**TAARIFA FUPI YA KIKUNDI CHA WANAWAKE – KIMBOLEMBOLE VICOBA KILICHOPO NYAMWAGE, KATA YA MBWARA WILAYA YA RUFIJI KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2017.**

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa ndugu Amour Hamad Amour; sisi akina mama wa Nyamwage tunakukaribisha kwenye kikundi chetu cha kuweka na kukopa (VICOBA). Aidha, tunakupongeza kwa jukumu kubwa la Kitaifa ulilonalo.

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge, Kikundi chetu kina jumla ya wanachama 13 ambao ni kinamama tuliojiunga na kuunganisha nguvu zetu kwa pamoja ili tuweze kukusanya mtaji kwa lengo la kujiongezea kipato na kujiajiri.

Kikundi chetu kinajishughulisha na VICOBA, ufugaji kuku wa kienyeji na kilimo cha bustani na matunda.

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge, tunapenda kuishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kwa ushirikiano wanaotupatia ikiwa ni ushauri pamoja na uwezeshaji kupitia Mfuko wa maendeleo ya wanawake (WDF) ambapo kwa mwaka 2015/2016 tumefanikiwa kupata mkopo wa Tsh 2,000,000.00 (milioni mbili tu) ambayo ilituwezesha kuongeza mtaji wetu na tumelipa zote lakini tumeahidiwa kukopeshwa tena mwaka huu na Halmashauri yetu.

Kwa sasa kikundi chetu kina Jumla ya Tsh 6,000,000.00 (milioni sita tu) ambazo zipo kwenye akaunti yetu ya Benki Na. 21310003257 Kimbolembole NMB Kibiti na fedha zingine tunatunzia kwenye sanduku letu la VICOBA tulilonalo hapa kijijini kwetu.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge, kwa heshima na taadhima tunakuomba utukagulie mradi wetu wa VICOBA.

Ni sisi kinamama wa Kimbolembole VICOBA Nyamwage.

***"Mwenge Oyee"***

**SALOME PASTORY MSURA**

**KATIBU WA KIKUNDI CHA KIMBOLEMBOLE**

**TAARIFA FUPI YA MRADI WA KILIMO CHA UFUTA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU TAREHE 03/06/2017 WILAYANI RUFIJI**

**Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru,** Ndg **Amour Hamad Amour**, kwa niaba ya wananchi wa kata ya Mbwara wilayani Rufiji naomba nichukue fursa hii kukupongeza kwa kupewa nafasi hii adimu ya kuwa kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa kwa mwaka huu.

**Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge**, mbele yako ni mradi wa shamba la kilimo cha Ufuta ambalo ndani yake kuna miche ya mikorosho ya kisasa. Shamba hili lina ukubwa wa ekari 100. Lakini katika msimu huu nimefanikiwa kulima ekari 57 ambapo nimepanda ufuta na miche 1,200 ya mikorosho.

**Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge**, nimeamua kujishughulisha na mradi huu ili kutekeleza kwa vitendo maagizo ya Serikali yanayotutaka sisi viongozi kuwa mfano kwa jamii katika kushiriki kwenye shughuli za Maendeleo. Lengo ni kuwahimiza vijana wenzangu kuachana na dhana potofu kuwa kilimo ni kwa wazee tu bali ni kwa wote. Pia, ajira si kufanya kazi Serikalini tu bali hata kilimo ni ajira na kinalipa. Aidha, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji (Idara ya Kilimo) kwa kunipatia mbegu bora za ufuta na miche bora ya mikorosho. Shamba hili limekuwa shamba darasa kwa wakulima wanaonizunguka.

**Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge**, shamba hili limegharimu kiasi cha Tsh. 25,000,000 hadi kufikia hatua hii. Matarajio ya mradi huu ni kupata faida ya Tsh.57,000,000/=, hivyo natarajia kuboresha maisha yangu na kununua zana bora za kilimo baada ya kuuza ufuta. Korosho zitaanza kuvunwa baada ya miaka minne.

**Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge,** pamoja na mafanikio ya mradi huu, nimekutana na changamoto kadhaa kama vile uwepo wa wanyama waharibifu wa mazao mfano nyani na matumizi duni ya zana za kilimo. Hatua nilzochukua kukabiliana na changamoto hizo ni kuweka ulinzi shambani kwa kuwafukuza wanyama waharibifu. Pia nimeshaomba mkopo wa trekta.

**Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge**, naomba nimalizie kwa kuiomba Serikali kuongeza kiwango cha mikopo kwa vijana ili waweze kuongeza vipato vyao. Mwisho natoa pongezi kwa kuchagua shamba langu kuwa ni sehemu ya kutembelewa na mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu na niwatakie safari njema.

***Mungu ibariki Tanzania, Mungu bariki Vijana , Mungu Ubariki Mwenge wa Uhuru.***

***Asanteni kwa kunisikiliza.***

***"Mwenge Oyee"***

***Juma Abdallah Ligomba***

***(Mkulima)***

**TAARIFA YA MRADI WA UJENZI WA OFISI YA KATA YA CHEMCHEM KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2017 WILAYANI RUFIJI TAREHE 03.06.2017**

Ndugu Amour Hamad Amour, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2017; Sisi wananchi wa Kata ya Chemchem tunayo furaha kuupokea Mwenge wa Uhuru katika Kata yetu. Tunakukaribisha wewe binafsi pamoja na msafara wako wote unaouongoza katika kufanikisha Mbio za Mwenge wa Uhuru 2017.

Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwaka 2014. Mradi huu utakapokamilika utagharimu jumla ya shilingi **40,000,000.00** Kwa kuchangiwa kama ifuatavyo:-

- Mchango wa Nguvu za wananchi Tshs. 3,500,000.00
- Mchango wa Halmashauri (W) Tshs. 36,500,000.00

**JUMLA** Tshs. **40,000,000.00**

Hadi hapa jengo lilipofikia limegharimu Tshs.23, 000,000.00. Kati ya hizo Tshs.4,600,000.00 ni mchango wa wananchi na Tshs.18,400,000.00 ni mchango wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji.

Kata hii inaundwa na vitongoji **7** yenye wakazi **5,133** ambao kati yao wanawake ni **2,687** na wanaume ni **2,446.**

Manufaa ya mradi huu utakapokamilika utawawezesha wakazi wa kata hii kupata huduma za kiutawala kwenye mazingira yaliyoboreshwa ikiwemo maadili na udhibiti wa rushwa.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017, karibu utuwekee jiwe la Msingi mradi wetu wa Ujenzi wa Ofisi ya Kata katika Kitongoji cha Kindwitwi.

***"MWENGE OYEE"***

***MAMLAKA YA MJI MDOGO WA UTETE OYEE!***

***UTAWALA BORA OYEEEE!***

***"Shiriki kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Nchi"***

***SUZAN THOMAS KAWIZA***

***AFISA MTENDAJI KATA***

***KATA YA CHEMCHEM***

**TAARIFA FUPI KUHUSU KIKUNDI CHA TUMAINI KITONGOJI CHA KINDWITWI KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2017**

1. **JINA LA KIKUNDI NI TUMAINI**
   Kikundi hiki kimeundwa na Wanakijiji wa Kindwitwi kwa lengo la kuelimisha Jamii. Kilianza kutambulika kwa jina la Upendo Group. Baada ya Kikao kilichofanyika tarehe 30/11/2014, Wanakikundi kwa maana ya Wajumbe waliamua kubadili jina la mwanzo na kukipa jina la **KIKUNDI CHA TUMAINI**.
2. **LENGO LA KIKUNDI CHA TUMAINI**
   Lengo la Kikundi cha Tumaini ni kutoa Elimu mahususi kuhusu Elimu ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi, Ukoma, Maambukizi ya Kifua Kikuu ikiwemo unyanyapaa kwa jamii katika rika zote.
   Mpango Mkakati wa kikundi ni kutoa uelewa kwa jamii kuhusu magonjwa haya hususani sehemu za Vijijini na pia kuondoa unyanyapaa kwa wale walio na maambukizi ya magonjwa mbalimbali. Ikumbukwe kuwa jamii hushindwa kujitokeza au kuweka wazi matatizo ya magonjwa waliyonayo na hata wakati mwingine kushindwa kuhudhuria vituo vya tiba.
3. Mnamo tarehe 22 Feb, 2015 kikundi hiki kilianza kutoa Elimu kwa njia ya Sinema, Elimu fupi ya maneno na Burudani ya Muziki kwa ajili ya kuelimisha wananchi.
4. Tunapenda kumshukuru mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Rufiji kwa kutuchangia fedha shilingi 800,000/= alipotutembelea Januari 2017 fedha zilizotusaidia usafiri wa kupita kwenye kampeni vijijini na kwenye kliniki za mama na mtoto kutoa elimu. Kipekee tunaomba kutoa shukurani kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kupitia Mganga Mkuu wa Wilaya kwa kututembelea mara kwa mara kutupa ushauri na kutuazimisha projekta pale ya kwetu inapokuwa imeharibika. Mwisho tunawapongeza wafadhili KLCCBA taasisi iliyobuni mawazo ya sisi kuanzisha kikundi na kutupa projekta ya kuanzia shughuli zetu.

**JUMLA YA WANAKIKUNDI CHA TUMAINI NI:-**

i. MUSA NGANYWAMA – MWENYEKITI
ii. MOZA KINDEKA – KATIBU
iii. MWARAMI NDETE – MJUMBE
iv. ALLY MKELE - MJUMBE
v. ASHURA NGOENGO - MJUMBE
vi. SHABANI ALLY - MJUMBE
vii. FRANK TAJI - MJUMBE

**Ni sisi wanakikundi cha Tumaini**

***"Mwenge wa Oyee"***

**MUSSA NGANYWAMA**

**MWENYEKITI WA KIKUNDI**

**TAARIFA FUPI YA MRADI WA UJENZI WA MADARASA, MABWENI NA VYOO KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2017**

Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa ndugu Amour Hamad Amour, mbele yako ni mradi wa ujenzi wa madarasa manne sambamba na ujenzi wa mabweni mawili, ujenzi wa vyoo matundu 14 na ukarabati wa bwalo la chakula na bweni moja ambayo ni miradi inayotekelezwa katika shule hii. Miradi hii kwa pamoja ina thamani ya Tshs. **264,157,189.00**. Kati ya hizo, Tshs. **259,000,000.00** ni fedha kutoka fungu la lipa kwa matokeo (P4R) Tsh. na Tsh. **5,157,189.00** ni mapato ya ndani ya Halmashauri. Fedha hii inafanya kazi kama ifuatavyo:-

(i) 80,000,000/= Ujenzi wa Madarasa manne (4) na samani zake
(ii) 150,000,000/= Ujenzi wa Mabweni mawili na utengenezaji wa vitanda 128
(iii)16,157,189/= Ujenzi wa vyoo matundu 14
(iv)18,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa jiko, Bwalo na Bweni moja

Kulingana na adhima ya Serikali ya kuwawezesha Vijana kujitegemea kiuchumi na kukuza pato la familia pamoja na kuwajengea uwezo wa kujitegemea, Halmashauri imetoa kipaumbele kwa vijana kufanya kazi zote za Ujenzi na ukarabati wa shule. Tunavyo vikundi vine vilivyosajiliwa na Halmashauri yetu na ndivyo vinavyofanya kazi ya ujenzi kwenye Miradi. Vikundi hivyo ni:

1. Lugongwe "Construction group" lenye vijana wenye fani ya Ujenzi, Ufundi Umeme, Mafundi bomba na Uselemala. Jumla vijana 28
2. Umoja ni nguvu, lenye vijana wa fani ya Ujenzi na fundi Bomba. Jumla vijana 22
3. Mnondo group lenye vijana wa fani za Ufundi Ujenzi, Umeme na Mafundi bomba. Jumla vijana 12
4. Mkela group lenye Vijana wenye fani za Ujenzi na Uselemala. Jumla vijana10.
   Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge, tunakuomba utuwekee jiwe la msingi katika mradi huu.

***"Mwenge Oyee".***

…………………………

***HILLARY BASA NGELA***
***MKUU WA SHULE***
***SHULE YA SEKONDARI UTETE***